**Tafsiri ya kitabu:**

al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah

**Mwandishi:**

Shaykh-ul-Islaaam Ibn Taymiyyah

**Chapa ya kwanza:**

Nakala 500

**Kimefasiriwa na:**

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

**Kimepitiwa na:**

Abu Bilaal ´Uthmaan Nu´umaan

**Wachapishaji wa kitabu:**

- Kina mama wa Denmark

- Faatwimah bint Khaliyfah bin Muhammad

**Haki Zote Zimehifadhi. Hairuhusiwi Kupiga Chapa Kitabu Hiki Kwa Jinsi Yoyote Ile Bila Idhini Ya Mfasiri**

**Utangulizi wa mpitiaji ........................................................................................ 4**

**Kuamini Majina na Sifa za Allaah........................................................................ 8**

**Kuamini yale Aliyojisifia Allaah Nafsi Yake Mwenyewe katika Kitabu Chake...... 9**
**Dalili ya Uhai wa Allaah ... 10**
**Dalili ya Elimu ya Allaah ... 10**
**Dalili ya Nguvu za Allaah ... 11**
**Dalili ya Kuona na Kusikia kwa Allaah ... 11**
**Dalilia ya Matakwa ya Allaah ... 12**
**Dalili ya Kupenda kwa Allaah ... 12**
**Dalili ya Kuridhia kwa Allaah ... 13**
**Dalili ya Wingi wa Huruma na Kurehemu kwa Allaah ... 14**
**Dalili ya Hasira na Kughadhibika kwa Allaah na kuchukia Kwake ndani ya Qur-aa na kwamba Yeye Allaah Amesifika kwa hilo ... 14**
**Dalili ya Kuwasili na Kuja kwa Allaah ... 15**
**Dalili ya Uso wa Allaah ... 16**
**Dalili ya Mikono ya Allaah ... 16**
**Dalili ya Macho ya Allaah ... 17**
**Dalili ya Kusikia na Kuona kwa Allaah ... 17**
**Dalili ya Adhabu na Njama za Allaah ... 18**
**Dalili ya Kusamehe, Kurehemu na Uwezo wa Allaah ... 19**
**Dalili ya Majina ya Allaah ... 20**
**Aayah zinazokanusha ulinganisho na ushirika pamoja na Allaah ... 20**
**Dalili ya kulingana kwa Allaah juu ya ´Arshi ... 22**
**Dalili ya kwamba Allaah Yuko juu ya viumbe Vyake ... 23**
**Dalili ya Allaah kuwa pamoja na viumbe Vyake kwa Ujuzi Wake ... 23**
**Dalili ya Maneno na Kuongea kwa Allaah ... 25**
**Dalili ya kwamba Qur-aan inatoka kwa Allaah ... 28**
**Dalili ya kwamba waumini watamuona Allaah siku ya Qiyaamah ... 28**
**Sifa za Allaah zimetajwa katika Sunnah ... 29**
**Dalili ya kwamba Allaah Huteremka katika mbingu ya chini ... 29**
**Dalili ya Kufurahi kwa Allaah ... 30**
**Dalili ya Kucheka kwa Allaah ... 30**
**Dalili ya Kustaajabu kwa Allaah ... 30**
**Dalili ya Mguu wa Allaah ... 30**

**Dalili ya Maneno na Sauti ya Allaah ..... 30**
**Dalili ya kwamba Allaah Yuko juu ya mbingu na Sifa zingine ..... 31**
**Dalili ya Allaah Kuwa pamoja na viumbe Vyake kwa Ujuzi wake ..... 32**
**Dalili ya Allaah kuwa mbele ya yule mwenye kuswali ..... 32**
**Dalili ya kwamba Allaah Yuko juu ya viumbe Vyake na Sifa zingine ..... 32**
**Dalili ya kwamba Allaah Yuko Karibu ..... 32**
**Dalili ya kwamba waumini watamuona Allaah siku ya Qiyaamah ..... 33**
**Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, watu wa kati na kati ..... 33**
**Kati ya Jahmiyyah na Mushabbihah ..... 33**
**Kati ya Qadariyyah na Jabriyyah ..... 34**
**Kati ya Murji-ah na Wa´iydiyyah ..... 34**
**Kati ya Haruuriyyah na Mu´tazilah na Murji-ah na Jahmiyyah ..... 34**
**Kati ya Rawaafidhw na Khawaarij ..... 34**
**Kuamini kuwa Allaah Yuko juu ya mbingu na juu ya ´Arshi na kwamba Yuko na viumbe Vyake ..... 34**
**Kuamini kuwa Allaah Yuko karibu na viumbe Vyake ..... 35**
**Kuamini kuwa Qur-aan inatoka kwa Allaah na haikuumbwa ..... 36**
**Kuamini kuwa waumini watamuona Allaah siku ya Qiyaamah ..... 36**
**Kuamini Aakhirah ..... 37**
**Hodhi (birika), Njia na Shafaa´ah ..... 38**
**Kuamini Qadar; kheri na shari yake ..... 39**
**Imani, matendo na kauli ..... 42**
**Mfumo sahihi kuhusiana na Maswahabah ..... 43**
**Kuamini karama za Mawalii ..... 48**
**Kufuata Njia ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah wake ..... 48**
**Sifa tukufu za Ahl-us-Sunnah ..... 49**
**Hitimisho ..... 51**

## Utangulizi wa mpitiaji

Himidi ni zake yeye Allaah (سبحانه وتعالى). Mwingi wa Rehmah mwenye kurehemu.

Swalah na salaam zimfikishie mbora wa viumbe, Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم), ahli zake, Maswahabah wake na kila mwenye kufuata mienendo yao. Amma ba´ad:

Hakika hiki ni kitabu kilichoandikwa kwa ufupi kubainisha I´tiqaad sahihi ya Al-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, kiitwacho "al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah" alichokiandika Shaykh-ul-Islaam Ahmad bin ´Abdil-Haliym bin ´Abdis-Salaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) alokufa mwaka 728 H.

Sababu ya kuandika kitabu hichi, alimjilia bwana mmoja alokuwa Qaadhiy katika mji wa Waasitw akamshtakia Shaykh-ul-Islaam uharibifu na upotofu uliopo katika mji wao katika upande wa I´tiqaad ya Majina ya Allaah na Sifa Zake. Akaandika kitabu hichi chenye kuzingatiwa kama tegemeo la msingi wa I´tiqaad sahihi ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah katika mambo ambayo waliyozama nayo watu katika Bid´ah.

Hakika ni kitabu ambacho kilichokusanya mfumo sahihi wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Jambo ambalo Muislamu siku zote hatosheki nalo, bali alihitajia siku zote katika maisha yake, kwa kwamba ´Aqiydah ndio msingi. Kitabu ambacho ni dalili tosha ya kuonesha umuhimu wake katika Ummah wa Kiislamu kwa kule kubahatika kupata Qabuul (kukubaliwa) kwa kushereheshwa na wanazuoni wa Kiislamu wa Ahl-us-Sunnah mbalimbali katika zama tofautitofauti, bali na kusomeshwa katika ulimwengu wa Kiislamu tokea zama hizo mpaka leo na mpaka ulimwengu utakapomalizika.

Na leo nazidi kumshukuru Allaah (سبحانه وتعالى) na kufurahi tena kwa kuwa kijana chetu mpendwa – Allaah Amuhifadhi – al-Akh Abu Bakr Khatwiyb. Amesimama na kukifasiri kitabu hichi kwa lugha ya Kiswahili ili mujtamaa wetu ufaidike na kujua misingi sahihi ya I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Allaah Ampe kula la kheri hapa duniani na huko Aakhirah na Aijaalie ´amali hii iwe Swadaqat-un-Jaariyah ya mzee wake alokwenda mbele ya haki. Allaah Amrahamu na Amuweke mahali pema. Na yeye ampe afya njema na Ikhlaasw na hima kuendelea kufanya kazi hii ya uandishi na nyinginezo za Da´wah ili mujtamaa wa Kiislamu unufaike na Amuwekee katika mizani ya hasanati zake.

*Wa SwallaAllaahu ´alaa Muhammad wa ´alaa alihi wa Aswhaabihi wa Sallam.*

### Dalili ya Wingi wa Huruma na Kurehemu kwa Allaah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

**"*BismiLLaahir-Rahmaanir-Rahiym* (Kwa Jina la Allaah Mwingi wa Rahmah, Mwenye kurehemu)."(27:30)**

رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَّحْمَةً وَعِلْمًا

**"Mola wetu! Umekienea kila kitu kwa Rahmah na elimu."(40:07)**

وَكَانَ بِالْمُؤْمِنِينَ رَحِيمًا

**"Na Yeye daima kwa Waumini ni *Rahiymaa* (Mwenye huruma)."(33:43)**

كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ

**"Mola wenu Amejiwajibishia juu ya Nafsi Yake Rahmah."(06:54)**

وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

**"Naye ni *Al-Ghafuwrur-Rahiym* (Mwingi wa kusamehe - Mwenye kurehemu)."(10:107)**

فَاللَّهُ خَيْرٌ حَافِظًا ۖ وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ

**"Basi Allaah ni *Khayrun-Haafidhwaa* (Mbora wa kuhifadhi). Naye ni *Arhamur-Raahimiyn* (Mbora wa kurehemu kuliko wanaorehemu)."(12:64)**

### Dalili ya Hasira na Kughadhibika kwa Allaah na kuchukia Kwake ndani ya Qur-aa na kwamba Yeye Allaah Amesifika kwa hilo

وَمَن يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُّتَعَمِّدًا فَجَزَاؤُهُ جَهَنَّمُ خَالِدًا فِيهَا وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَلَعَنَهُ وَأَعَدَّ لَهُ عَذَابًا عَظِيمًا

**"Na atakayemuua Muumini kwa kusudi, basi jazaa yake ni (Moto wa) Jahannam, atadumu humo milele na Allaah Atamkasirikia na**

Kamwambia hali kadhalika ami yake Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) ambaye alikuwa amekuja kushtaki ya kwamba baadhi ya Quraysh wanawachukia Banuu Haashim. Akasema:

"Ninaapa kwa Yule ambaye Nafsi yangu iko Mkononi Mwake. Hawatoamini mpaka wawapende kwa ajili ya Allaah na kwa ukaribu[65] wenu kwangu."[66]

Na akasema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Allaah Kawachagua Banuu Ismaa´iyl. Na kutoka Banuu Ismaa´iyl Kachagua Kanaanah. Na kutoka Kanaanah Kachagua Quraysh. Na kutoka Quraysh Kachagua Banuu Haashim na Kanichagua mimi kutoka Banuu Haashim."[67]

Hali kadhalika wanawapenda na kufanya urafiki na wake za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), wao ni wamama wa waumini. Na wanaamini ya kwamba wao ndio wake zake Aakhirah, na hususan Khidiyjah (Radhiya Allaahu ´anha) ambaye ni mama wa watoto wake wengi. Na yeye ndiye alikuwa wa kwanza kumuamini na kumsaidia kwa kazi yake na alikuwa ni mwenye manzilah ya juu kwake.

Na asw-Swiddiyqah bint asw-Swiddiyq (Radhiya Allaahu ´anhumaa),[68] ambaye kasema Mtume kuhusu yeye:

"Ubora wa ´Aaishah kwa kulinganisha na wanawake wengine ni kama ubora wa Thariyd[69] kulinganisha na chakula kingine."[70]

Na wanajiweka mbali na njia ya Rawaafidhw, ambao wanawachukia na kuwatukana Maswahabah, hali kadhalika Nawaasib, ambao wanawaudhi Ahl-ul-Bayt, aidha kwa kauli au matendo.

Na wanayanyamazia yaliyopitika baina ya Maswahabah na wanasema:

---

na thawabu Zake ikiwa mtawap haki zao." (Sharh al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah, mjaladi. 2, uk. 275, iliotolewa na Daar Ibn-ul-Jawziy)

[65] Yaani na kwa kuwa nyinyi ni familia yangu

[66] Ahmad katika "Fadhwaail-us-Swahabah" (1756).

[67] Muslim (2276).

[68] ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anha)

[69] Ni mkate uliokuwa ukionekana ni mtamu sana wakati huyo unaowekwa kwenye mchuzi wa nyama

[70] al-Bukhaariy (3770) na Muslim (2446).

